
# Kiswahili

## KITABU CHA MWANAFUNZI

### Darasa la Tatu




Taasisi ya Elimu Tanzania

*Mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hakiuzwi*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Kiswahili

## Kitabu cha Mwanafunzi

## Darasa la Tatu


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 13

Jina la Chapisho: Kiswahili Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tatu

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978 - 9976 - 61 - 713 - 9

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 19 Mwezi Januari Mwaka 20 18 kuwa kitabu cha Kiada kwa ajili ya Darasa la Tatu katika ngazi ya elimu ya Msingi nchini Tanzania kulingana na Muhtasari wa mwaka 2016.

**Dkt. Edicome Cornel Shirima**
Kaimu Kamishna wa Elimu.

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2018

Toleo la Kwanza 2018
Chapa ya Pili 2021

ISBN 978 - 9976 - 61 - 713 - 9

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P 35094
Dar es Salaam

Simu: +255 735 041 170 / +255 735 041 168
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kupiga chapa, kutafsiri wala kukitoa kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi ya Taasisi ya Elimu Tanzania.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 2 23/07/2021 14:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Yaliyomo

**Utangulizi**........................................ v

**Shukurani**........................................ vi

**Sura ya Kwanza**
Sauti zinazounda maneno........................................ 1

**Sura ya Pili**
Matamshi ya herufi........................................ 8

**Sura ya Tatu**
Kuzungumza........................................ 15

**Sura ya Nne**
Ufahamu........................................ 24

**Sura ya Tano**
Kuandika kwa usahihi........................................ 29

**Sura ya Sita**
Taarifa za matukio mbalimbali........................................ 38

**Sura ya Saba**
Kuelezea wanyama na wadudu........................................ 49

**Sura ya Nane**
Kuelezea mahali vilipo vitu na watu........................................ 57

**Sura ya Tisa**
Siku za juma........................................ 65

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Sura ya Kumi**
Uhusiano wa watu katika familia........................................ 69

**Sura ya Kumi na Moja**
Shughuli za kila siku........................................................ 72

**Sura ya Kumi na Mbili**
Maneno yenye maana sawa na kinyume chake.................... 76

**Sura ya Kumi na Tatu**
Ndege wetu............................................................... 87

**Sura ya Kumi na Nne**
Shairi.................................................................... 93

**Sura ya Kumi na Tano**
Matumizi ya kamusi........................................................ 97

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 4 23/07/2021 14:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Utangulizi

Kitabu hiki kitakujengea uwezo wa kuzungumza, kutambua sauti zinazounda maneno na kusoma kwa ufasaha. Aidha, kitakujengea uwezo wa kusoma kwa ufahamu na kutumia msamiati.

Kitabu kina mazoezi mbalimbali yatakayokuwezesha kujenga ujuzi uliokusudiwa. Vilevile, kitakuwezesha kupima uelewa wako katika kila sura utakayojifunza.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 5 23/07/2021 14:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki waliofanikisha uandishi na maandalizi ya kitabu hiki.

TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wote walioshiriki kutayarisha kitabu hiki wakiwemo wachapaji, wasanifu, wahariri, wachoraji na wapiga chapa. Pia, inatoa shukurani kwa shule zote zilizoshiriki katika ujaribishaji wa maudhui na uhariri wa kitabu hiki.

Aidha, Taasisi inatoa shukurani za pekee kwa Shirika la “Global Partnership for Education (GPE)” kupitia Mradi wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) uitwao “Literacy and Numeracy Education Support (LANES)” kwa ufadhili wao uliofanikisha kazi ya kutayarisha na kuchapa kitabu hiki.

Mwisho, Taasisi inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kusimamia kwa ukaribu zoezi zima la uandishi wa kitabu hiki.



**Dkt. Aneth A. Komba**
**Mkurugenzi Mkuu**
***Taasisi ya Elimu Tanzania***

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 6 23/07/2021 14:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kwanza

## Sauti zinazounda maneno

Ukijifunza sura hii utaweza kusoma silabi na maneno yenye sauti za herufi **gh, py, nz, sw, lw, ky, tw, ng'w, nyw** na **shw**. Huu ni mwendelezo wa sauti za herufi ulizojifunza darasa la pili.

Kusoma na kuandika maneno yenye sauti za herufi **gh, lw, py, nz, sw** na **tw.**

Soma kwa sauti maneno haya.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| (a) ghali | (b) Kulwa | (c) nzi | (d) swali | (e) twanga |
| (f) mpya | (g) gharama | (h) Kilwa | (i) nzige | (j) swala |
| (k) tweta | (l) jipya | (m) ghairi | (n) Nzega | (o) swaga |
| (p) kutwa | | | | |

Soma habari hii, kisha jibu maswali yanayofuata.

### Darasa jipya

Neema na **Kulwa** ni marafiki. Wote wanasoma katika Shule ya Msingi Mkwajuni. Mwaka jana walikuwa darasa la pili. Mwaka huu wameingia darasa la tatu. Shule ya Msingi **Mkwajuni** ilifunguliwa wiki ya **kwanza** ya mwezi Januari. Siku ya kufungua shule **wanafunzi** wote walifika shuleni mapema. Walifanya usafi wa mazingira ya shule, kisha wakasimama mstarini.

**Swaiba** alikuwa mwalimu wa zamu. Aliwasalimia wanafunzi na kuwatakia heri ya mwaka **mpya**. Aliwaeleza kuwa kila




Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 1 23/07/2021 14:18

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mwanafunzi **anapaswa** kusoma kwa bidii. Aidha, anapaswa kuzingatia sheria za shule. Aliwaeleza wanafunzi kuwa vyumba vya madarasa vimebadilika. Wanafunzi waliokuwa darasa la kwanza mwaka uliopita, wataingia chumba cha darasa la pili. Wanafunzi waliokuwa darasa la pili wataingia chumba cha darasa la tatu. Baada ya matangazo, wanafunzi waliingia madarasani.

Wanafunzi wa darasa la tatu **walianza** mwaka wakiwa na furaha. Kila mwanafunzi alikuwa na hamu ya kuanza kusoma katika darasa **jipya**. Walipoingia darasani, mwalimu wa darasa aliwaongoza kuchagua viongozi. Neema alichaguliwa kuwa dada wa darasa na **Ghalibu** kuwa kaka wa darasa.






FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maswali

1. Rafiki yake Neema anaitwa nani?
2. Neema na rafiki yake wanasoma shule gani?
3. Nani alikuwa mwalimu wa zamu?
4. Kwa nini wanafunzi wa darasa la tatu walikuwa na furaha?

## Zoezi la 1

1. Soma kwa sauti maneno yaliyokolezwa wino katika habari uliyosoma.
2. Unganisha sauti za herufi **gh lw py nz sw tw** na **a e i o u** kuunda silabi.

   **Mfano**

   Ukiunganisha sauti ya herufi **gh** na sauti ya herufi **a** unaunda silabi **gha**

   | | | | |
   |---|---|---|---|
   | (a) | gh | a | gha |
   | (b) | lw | - | - |
   | (c) | nz | - | - |
   | (d) | sw | - | - |
   | (e) | tw | - | - |

3. Tenganisha silabi zilizounda maneno.

   **Mfano**

   | | | | | |
   |---|---|---|---|---|
   | wanafunzi | wa | na | fu | nzi |
   | waliaswa | wa | li | a | swa |

   (a) walianza

   (b) jipya

   (c) anapaswa

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. Tenganisha sauti za herufi katika silabi.

**Mfano**

| | | | |
|---|---|---|---|
| | pya | py | a |
| (a) | swa | - | - |
| (b) | nzu | - | - |
| (c) | ghi | - | - |
| (d) | lwa | - | - |
| (e) | twe | - | - |

## Zoezi la 2

Soma maneno yafuatayo kwa sauti.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| (a) ghala | (b) ghorofa | (c) funza | (d) kwanza | (e) panzi |
| (f) nzi | (g) kanzu | (h) kitanzi | (i) nzige | (j) swali |
| (k) sweta | (l) swala | (m) mswaki | (n) jipya | (o) mpya |
| (p) upya | (r) Kilwa | (s) Kulwa | (t) twanga | (u) tweta |
| (v) twiga | (w) twisha | (y) patwa | (z) kutwa | |

## Zoezi la 3

Soma sentensi zifuatazo kwa sauti.

(a) Mwalimu amewauliza wanafunzi maswali.

(b) Baba amenunua nguo kwa bei ghali.

(c) Mwanafunzi ameanza kwenda shuleni.

(d) Huu ni mwaka mpya.

(e) Mjomba amejenga nyumba ya ghorofa.

(f) Kilwa ni mji mzuri.

(g) Kaka yake Kulwa anaitwa Mpetwa.



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 4 23/07/2021 14:18

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4

Tunga sentensi mbili kwa kila neno.

(a) mpya (b) ghali (c) swali (d) nzuri (e) Kulwa

Soma mazungumzo kati ya Sungura na Chui, kisha fanya mazoezi.



| | |
|---|---|
| **Sungura** | Habari za leo kaka Chui. |
| **Chui** | Nzuri! |
| **Sungura** | Leo umekunywa maji? |
| **Chui** | Sijanywa maji. |
| **Sungura** | Ooh! itabidi nimuagize Pweza atuletee maji kutoka baharini, "Leo bahari ni shwari". |



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| | |
|---|---|
| **Chui** | Hapana! Kuna binadamu anayeitwa Ng'wale anauza maji. |
| **Sungura** | Inaonekana humpendi Pweza. |
| **Chui** | Si kweli! Sina uadui na Pweza. |
| **Sungura** | Nafikiri tuwaache wote. Tuagize maji kutoka kwa Kyando. |
| **Chui** | Nakubaliana na wewe. Maji anayouza Kyando ni safi sana. |
| **Sungura** | Kweli! Itabidi tununue hayo. |
| **Chui** | Sawa mdogo wangu. |

## Zoezi la 5

Andika maneno yenye sauti za herufi zifuatazo kutokana na mazungumzo uliyoyasoma.

(a) ky (b) pw (c) ng'w (d) nyw (e) shw (f) nz

## Zoezi la 6

1. Tafuta maneno yenye sauti za herufi **nyw shw pw nz** tofauti na mazungumzo uliyosoma.

**Mfano**

**nyw** - nywele

**(a)** **shw** -

**(b)** **pw** -

**(c)** **nz** -

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Soma kwa sauti silabi hizi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **(a) pwa** | **(b) kya** | **(c) ng'wa** | **(d) pwi** |
| **(e) nywa** | **(f) shwi** | **(g) kye** | **(h) shwa** |
| **(i) ng'wi** | **(j) Kyo** | **(k) ng'we** | **(l) nywe** |

3. Soma kwa sauti sentensi hizi.
   (a) Bibi yangu anaishi Kyela.
   (b) Baba anapenda kula pweza.
   (c) Mzee Ng'wandu amejenga nyumba nzuri.
   (d) Hali ya bahari ni shwari.

## Zoezi la 7

Andika maana za maneno yafuatayo kwa kuchagua jibu sahihi.

**Mfano**
shwari – hali ya utulivu.

| Maneno | Maana |
|---|---|
| (a) shwari - | (i) kamba au uzi uliofungwa kwa duara |
| (b) ghali - | (ii) yenye bei kubwa |
| (c) pweza - | (iii) hali ya kutendeana ubaya baina ya watu |
| (d) kitanzi - | (iv) kiumbe wa baharini |
| (e) uadui - | (v) hali ya utulivu |

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 7 23/07/2021 14:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


# Sura ya Pili

## Matamshi ya herufi

Katika sura hii utajifunza kutamka, kusoma na kuandika maneno yenye sauti za herufi **s** na **th, z** na **dh, l** na **r, g** na **gh** kwa usahihi.

Kutamka maneno yenye sauti za herufi **s** na **th** kwa usahihi.

Tazama picha na namba zifuatazo, kisha fanya zoezi linalofuata.

1. 

2. 

3. 

4. 

5. 

6. **80**

7. **30**

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 8 23/07/2021 14:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1

1. Tamka majina ya vitu unavyoviona katika picha namba 1 hadi 5.
2. Tamka kwa sauti namba 80 na 30
3. Taja sauti ya mwanzo inayosikika unapotamka maneno samaki, sabuni, sarafu na saa.
4. Taja sauti ya mwanzo inayosikika unapotamka namba 80 na 30.

## Zoezi la 2

Soma maneno yafuatayo kwa sauti.

| | | | |
|---|---|---|---|
| (a) saa | (b) sahani | (c) subiri | (d) soko |
| (e) safari | (f) sabuni | (g) saruji | (h) msumari |
| (i) usafi | (j) pasi | (k) fenesi | (l) msusi |
| (m) thelathini | (n) themanini | (o) thamani | (p) thubutu |
| (r) theluji | (s) urithi | | |

## Zoezi la 3

Nakili sentensi zifuatazo katika daftari lako. Kisha chagua neno sahihi kwa kupigia mstari.

**Mfano**
(<u>Samaki</u>, thamaki) ni chakula bora.


(a) Mimi ninaoga kwa kutumia maji safi na (sabuni, thabuni).
(b) Juma anaishi karibu na (thoko, soko).
(c) Mwanafunzi mtiifu amepata alama (semanini, themanini).
(d) Mimi ninapenda kula (fenesi, fenethi).
(e) Bibi huosha (sahani, thahani) kabla ya kuweka chakula.


FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kutamka maneno yenye sauti za herufi **z** na **dh** kwa usahihi.

Tazama picha zifuatazo, kisha fanya zoezi.

1. 

2. 

## Zoezi la 4

1. Tamka majina ya vitu unavyoviona katika picha namba 1 na 2.
2. Taja sauti ya mwanzo inayosikika unapotamka maneno haya.
   (a) zawadi zulia zahanati zeze zao zabibu
   (b) dharau dhaifu dhoofu dhoruba

## Zoezi la 5

Soma kwa sauti maneno haya.

| | | | |
|---|---|---|---|
| (a) ziwa | (b) mnazi | (c) zeze | (d) zizi |
| (e) zuia | (f) nazi | (g) zito | (h) zamani |
| (i) mzazi | (j) maziwa | (k) dhoofu | (l) dharura |
| (m) madhara | (n) dhahabu | (o) adhabu | (p) dhambi |
| (r) dhuru | (s) dhuluma | (t) dhoruba | (u) dharau |



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 10 23/07/2021 14:18

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 6

Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kuchagua neno sahihi.

**Mfano**

**Dhahabu** hupatikana Tanzania.(zahabu, dhahabu)

1. Mimi ninapenda kupiga ______________. (dheze, zeze)
2. Gunia lililojaa viazi ni ______________ . (dhito, zito)
3. Pamba ni ______________ la biashara. (zao, dhao)
4. Mama alisema kuwa kuiba ni ________ . (dhambi, zambi)
5. Juma alikwenda kuwatembelea ____________ wake. (wadhazi, wazazi)

Kutamka maneno yenye sauti za herufi **l** na **r** kwa usahihi.

## Zoezi la 7

Soma kwa sauti maneno haya.

| | | | |
|---|---|---|---|
| (a) ladha | (b) lazima | (c) linda | (d) lala |
| (e) lami | (f) elea | (g) lima | (h) mali |
| (i) liza | (j) alika | (k) kalia | (l) koroboi |
| (m) barabara | (n) ridhia | (o) redio | (p) rika |
| (r) jeraha | (s) raba | (t) robo | (u) rudi |
| (v) bure | (w) roho | (y) ruhusa | (z) riadha |

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 11 23/07/2021 14:18



FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


## Zoezi la 8


Tazama picha zifuatazo, kisha tunga sentensi mbili kwa kila picha.


**Mfano**

1. Huu ni mlango.
2. Nyumba yetu ina mlango mzuri.







## Zoezi la 9

1. Andika maneno yafuatayo kwa usahihi.

   **Mfano**

   zuli – zuri

   (a) bule .......... (b) ria ..........
   (c) rami .......... (d) ledio ..........
   (e) luhusa .......... (f) balabala ..........
   (g) loho .......... (h) jelaha ..........

2. Soma kwa sauti maneno uliyoandika katika swali la kwanza.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kutamka maneno yenye sauti za herufi **g** na **gh** kwa usahihi.

## Zoezi la 10

Soma kwa sauti maneno haya.

| | | | |
|---|---|---|---|
| (a) gari | (b) gauni | (c) ugali | (d) fagio |
| (e) gego | (f) gitaa | (g) goti | (h) gunia |
| (i) guta | (j) ugua | (k) ghali | (l) ghala |
| (m) lugha | (n) ghorofa | (o) gharama | |

## Zoezi la 11

Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia herufi **g** au **gh.** Kisha soma kwa sauti maneno haya.

| | | |
|---|---|---|
| (a) – a r i | (b) – a l i | (c) l u – a |
| (d) – u n i a | (e) – o g o | (f) – a r a m a |
| (g) u – u a | (h) – a l a | (i) – a s i a |
| (j) – o t i | (k) – itaa | (l) – orofa |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 12

1. Nakili jedwali la maneno yafuatayo katika daftari lako. Kisha weka alama ya vema ( ✓) kwa kila neno sahihi na kosa ( ✗ ) kwa neno lisilo sahihi.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| samaki | zawadi | saruji | dhiwa | subiri |
| thoko | ziwa | sabuni | gali | sukari |
| gorofa | dhambi | ruka | ledio | lugha |
| dhulumu | thamaki | ulithi | rara | luhusa |

2. Orodhesha maneno yote yasiyo sahihi kutoka katika jedwali la swali la kwanza. Yaandike maneno hayo kwa usahihi.

**Mfano**

ledio – redio

(a) ............. - ............. (e) ............. - .............

(b) ............. - ............. (f) ............. - .............

(c) ............. - ............. (g) ............. - .............

(d) ............. - ............. (h) ............. - .............

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tatu


## Kuzungumza


Ukijifunza sura hii utaweza kuelezea vitu mbalimbali katika hali ya umoja na wingi. Vilevile, utaweza kutumia methali na nahau katika mazungumzo. Aidha, utaweza kusimulia hadithi.

Kuelezea vitu mbalimbali katika **umoja** na **wingi.**


Tazama picha zifuatazo, kisha fanya zoezi.


1.





2.






FOR ONLINE USE ONLY


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


3.






4.





5.





FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1

(a) Taja mahali vinapopatikana vitu katika picha namba 1 hadi 4.

**Mfano** Namba 4 machungwa yanapatikana sokoni.

(b) Taja majina ya vitu hivyo katika umoja na wingi.

**Mfano** kiti - viti.

(c) Eleza matumizi ya vitu vilivyopo katika picha namba 1 hadi 4.

**Mfano** kiti hutumika kukalia.

## Zoezi la 2

1. Taja vitu vitano vinavyopatikana shuleni.
2. Taja majina ya vitu hivyo katika umoja na wingi.
3. Eleza matumizi ya kila kimoja.

## Zoezi la 3

Taja wingi wa vitu hivi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| (a) gari | (b) simu | (c) jembe | (d) mti |
| (e) wembe | (f) sufuria | (g) chupa | (h) koti |
| (i) shati | (j) gauni | (k) mchanga | (l) jiwe |
| (m) nyumba | (n) nywele | (o) taa. | |

Taja umoja wa vitu hivi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| (a) mayai | (b) miti | (c) mifuko | (d) mabegi |
| (e) maini | (f) maembe | (g) miguu | (h) macho |
| (i) mabega | (j) vidole | (k) maji | (l) unga |
| (m) maziwa. | | | |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4

Badili sentensi zifuatazo ziwe katika wingi.

**Mfano**

1. Rangi **hii** ni nzuri.

   Rangi **hizi** ni nzuri.

2. Dawati **hili** limevunjika.
   Madawati **haya** yamevunjika.

(a) Mfuko huu ni mkubwa.
(b) Meza hii ni safi.
(c) Nyumba hii ni nzuri.
(d) Kitabu hiki ni kidogo.
(e) Jiwe hili ni kubwa.

## Zoezi la 5

Badili sentensi zifuatazo ziwe katika umoja.

**Mfano**

1. Furaha amepewa zawadi za **madaftari**.

   Furaha amepewa zawadi ya **daftari**.

2. Walimu **wanafundisha** vizuri.
   Mwalimu **anafundisha** vizuri.

(a) Miti mirefu imeanguka.
(b) Baba amenunua magari mawili.
(c) Wanafunzi wamepanda maua mazuri.
(d) Madarasa yetu yana madirisha makubwa.
(e) Taa za shule yetu zinawaka vizuri.


FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kutumia methali katika mazungumzo


Soma na igiza mazungumzo yafuatayo na wenzako.

1.




Mimi ni bomba.
Ninatoa maji ambayo yana matumizi mengi.
Ninajua methali isemayo **ndondondo si chururu.**

2.



Mimi ni ndoo. Ninaweza kuwekewa maji mengi.
Ninajua methali isemayo **maji yakimwagika hayazoleki**.

3.



Sisi ni nyuki.
Tunaishi kwenye mzinga.
Tunatengeneza asali tamu sana. Tunajua methali isemayo **fuata nyuki ule asali**. Lakini ukituchokoza tunakuuma.


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4.



Mimi ni Nyegere.
Ni mnyama mdogo.
Ninapenda sana kula asali.
Ninajua maana ya methali fuata nyuki ule asali. Maana yake, **fuata wema upate mema**. Mimi hutembelea maeneo yenye asali. Ushuzi wangu huwalevya nyuki.

5.



Mimi ni Sungura.
Ni mnyama mjanja kuliko wote. Ninajua methali isemayo **asiyesikia la mkuu huvunjika guu**.

6.



Mimi ni Fisi. Ni bwana afya wa porini. Ninajua maana ya methali asiyesikia la mkuu huvunjika guu.
Maana yake, **asiyesikia anayoambiwa na wakubwa mwisho hupata matatizo**.
Kutokana na uroho wangu mara nyingi napata matatizo makubwa.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 6

Malizia methali zifuatazo kwa kuchagua jibu sahihi kwenye kisanduku.

| | | |
|---|---|---|
| (i) hajikwai | (ii) haiozi | (iii) yaumiza matumbo |
| (iv) hula mbivu | (v) arobaini | (vi) haina baraka |
| (vii) si ujinga | | |

**Mfano**

Ngojangoja yaumiza matumbo.

(a) Mvumilivu ..................
(b) Kuuliza ..................
(c) Mwenda pole ..................
(d) Siku za mwizi ni ..................
(e) Akiba ..................
(f) Haraka haraka.....................

## Zoezi la 7

Toa maana ya nahau zilizopigiwa mstari kwa kuchagua jibu sahihi kwenye kisanduku.

| | | | |
|---|---|---|---|
| (i) mchoyo | (ii) mwizi | (iii) kuoa | (iv) kulewa pombe |
| (v) kushirikiana | (vi) kufa moyo | (vii) kukubaliana | (viii) amua |

**Mfano**

Baada ya kusubiri kwa muda mrefu <u>alikata shauri</u> kuondoka.
Kata shauri maana yake ni amua.

(a) Kaka <u>amepata jiko</u>.
(b) Mjomba <u>amevaa miwani</u>.
(c) Juma ana <u>mkono mrefu.</u>
(d) Wanakijiji wanafanya kazi <u>bega kwa bega</u>.
(e) Sara ana <u>mkono wa birika</u>.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kusimulia hadithi

Jibu maswali haya.

1. Je, ulishawahi kusimulia au kusimuliwa hadithi?
2. Kama ulisimuliwa, nani alikusimulia hadithi hiyo?
3. Hadithi hiyo ilikuwa inahusu nini?
4. Hadithi hiyo ilikuwa na mafunzo gani?

### Zoezi la 8

Tazama picha hizi, kisha jibu maswali.

1.



2.







Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 22 23/07/2021 14:18

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3.


4.


5.


6.


(a) Andika hadithi fupi.

Siku moja Bibi ______________________

(b) Soma kwa sauti hadithi uliyoandika.

(c) Hadithi uliyoandika inatufundisha nini?

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 23 23/07/2021 14:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nne

## Ufahamu

Ukijifunza sura hii utaweza kusoma kifungu cha habari. Aidha, utajibu maswali kutokana na habari uliyoisoma. Vilevile, utaweza kutunga na kuandika sentensi kwa usahihi.

### Kusoma kifungu cha habari

Soma habari hii, kisha jibu maswali.

#### Mtoto mwema

Fikiri ni mwanafunzi wa darasa la tatu. Anasoma katika Shule ya Msingi Jitegemee. Fikiri ana dada mmoja na kaka wawili. Yeye ni kitindamimba katika familia yao. Fikiri anaishi na shangazi yake katika mkoa wa Arusha. Shangazi yake anaitwa Neema.


Fikiri anampenda sana shangazi yake. Humsaidia kazi za nyumbani kama vile kuosha vyombo, kufua na kufagia. Vilevile, humwagilia bustani ya maua. Nyumba yao inapendeza sana.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 24 23/07/2021 14:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Fikiri anapokuwa shuleni, husoma kwa bidii. Anajua kusoma, kuandika na kuhesabu. Huwasaidia wanafunzi wenzake ambao huhitaji msaada. Rafiki yake Fikiri anaitwa Tumaini. Tumaini alikuwa hawezi kuhesabu vizuri lakini Fikiri alimsaidia. Siku hizi Tumaini anaweza kuhesabu vizuri. Walimu na wanafunzi wanampenda sana Fikiri.

Pia, Fikiri ni mwanafunzi mtiifu. Hutekeleza maelekezo anayopewa na wazazi au walezi na hata wanafunzi wenzake. Akiwa shuleni huwaheshimu walimu na viongozi wote wa shule. Fikiri ni mfano bora wa kuigwa.

Siku moja, Fikiri alikuwa anatoka shuleni kuelekea nyumbani. Njiani alikutana na bibi mmoja. Bibi alikuwa amebeba kuni kichwani na kikapu mkononi. Fikiri alimsalimia kisha akamwambia, "Bibi naomba nikusaidie kubeba kikapu".

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Bibi alifurahi sana. Akajibu salamu na kumpa kikapu kisha wakaendelea na safari. Walipofika njiapanda Fikiri akamwambia bibi, "Mimi ninaelekea barabara iendayo kulia". Bibi akamwambia Fikiri, "Asante sana mjukuu wangu. Mimi naelekea barabara iendayo kushoto". Bibi alichukua kikapu chake na kumshukuru Fikiri. Kisha kila mmoja aliendelea na safari yake.

## Zoezi la 1

Jibu maswali haya.

1. Fikiri anasoma shule gani?
2. Nani alimsaidia Tumaini kujua kuhesabu?
3. Kwa nini Fikiri ni mfano wa kuigwa?
4. Kwa nini bibi alimshukuru Fikiri?
5. Habari hii inatufundisha nini?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2

Andika **NDIYO** kwenye sentensi ya kweli au **HAPANA** kwenye sentensi isiyo ya kweli.

1. Wanafunzi hawapaswi kuwasaidia wazazi wao kazi za nyumbani..................
2. Wanafunzi wanaweza kufundishana..................
3. Fikiri ni mtoto mwenye tabia nzuri..................
4. Hatupaswi kuiga tabia ya Fikiri..................
5. Fikiri ni mwanafunzi mtiifu..................
6. Bibi alimsifu Fikiri kwa tabia yake mbaya..................
7. Fikiri ni mfano bora wa kuigwa..................
8. Shangazi ni ndugu wa kike wa baba..................

## Zoezi la 3

Chagua jibu sahihi na kuliandika sehemu iliyoachwa wazi.

1. Fikiri ni kitindamimba katika familia yao. Maana yake ni.......................
   (a) mtoto wa kwanza kuzaliwa
   (b) mtoto wa pili kuzaliwa
   (c) mtoto wa mwisho kuzaliwa
   (d) mtoto wa kati kuzaliwa

2. Mwanafunzi mtiifu maana yake ni........................
   (a) mwenye kutekeleza yale anayoambiwa
   (b) asiyependa kutumwa
   (c) anayeongea sana
   (d) anayechokoza wenzake

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Kutoa msaada maana yake ni.....................
   (a) kumpa mtu zawadi
   (b) kumpongeza
   (c) kumsaidia mtu kuondoa shida au tatizo lake
   (d) kumpa mtu pesa ili asirudie kuomba tena
4. Shangazi ni.............................
   (a) kaka yake mama
   (b) dada yake baba
   (c) mdogo wake dada
   (d) mdogo wake kaka

## Zoezi la 4

1. Soma sentensi zifuatazo kwa umakini, kisha pigia mstari neno lililokosewa.
   (a) Fikiri ni wanafunzi wa darasa la tatu.
   (b) Watoto anapaswa kuwaheshimu wazazi.
   (c) Mwanafunzi wamefungua shule.
   (d) Dada na kaka anaimba wimbo.
   (e) Bibi walikuwa amebeba kuni na kikapu.
2. Andika sentensi za swali la kwanza kwa usahihi.

## Zoezi la 5

Tunga sentensi moja kwa kila neno.

| | | |
|---|---|---|
| (a) msaada | (b) bidii | (c) mwema |
| (d) tabia | (e) mtiifu | |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tano

## Kuandika kwa usahihi

Ukijifunza sura hii utaweza kuandika sentensi, habari na hadithi fupi. Vilevile, utaweza kutumia alama hizi . , ! ? na " " kwa usahihi.


Kutumia alama hizi . , ! ? na " " katika sentensi.

Jibu maswali haya.

1. Taja majina ya alama hizi . , ! ? " "
2. Alama hii , inatumika wapi?

Angalia picha, kisha soma sentensi kwa sauti. Chunguza matumizi ya alama katika sentensi hizo.

1.






Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 29 23/07/2021 14:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2.





3.




FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4.




5.



Dada amebeba nanasi, embe, ndizi na zabibu.

## Zoezi la 1

1. Taja alama za uandishi unazoziona katika sentensi zinazoonekana katika picha namba 1 hadi 5.

**Mfano**

Sentensi kwenye picha ya kwanza imetumia **kituo kikubwa.**

2. Alama ya kituo kikubwa hutumika wapi?



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 31 23/07/2021 14:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2


Soma na igiza.

1.



Mimi ni **nukta**. Kwa jina lingine ni kituo kikubwa. Ninatumika mwishoni mwa sentensi. Alama yangu ni hii **.**

2.



Mimi ni **mkato**. Watu wengi huniita kituo kidogo. Ninatumika kutenganisha vitu vilivyoorodheshwa kwa mfululizo. Alama yangu ni hii **,**

3.



Mimi ni **mshangao.**
Watu hunitumia kila wanaposhangaa. Alama yangu ni hii **!**

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4.





Mimi ni **kiulizo**. Ninatumika kila linapoulizwa swali. Alama yangu ni hii **?**

5.




Mimi ni **fungua na funga semi**. Ninatumika kuonesha maneno halisi ya mzungumzaji. Alama zangu ni hizi **“ ”**.

6.




Mimi ni **herufi kubwa**. Watu hunitumia sana mwanzoni mwa majina yao. Hunitumia mwanzoni mwa majina ya miji, watu au majina ya mahali. Vilevile, hunitumia mwanzoni mwa sentensi. Mimi nina sura tofauti kwa kila herufi. Baadhi ya sura zangu ni **A B CH D E F**

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kutumia alama hizi . , ! ? na " " katika habari na hadithi.

## Zoezi la 3

Weka alama hizi . , " " na ! kwa usahihi mbele ya jina la alama.

**Mfano**

Kituo kikubwa .

| Jina | Alama |
|---|---|
| (a) Mkato | ______ |
| (b) Mshangao | ______ |
| (c) Kiulizo | ______ |
| (d) Fungua na funga semi | ______ |
| (e) Kituo kikubwa | ______ |

## Zoezi la 4

Andika sentensi zifuatazo kwa usahihi. Hakikisha unaweka alama sahihi za uandishi na herufi kubwa.

1. sebo anaishi mkoa wa morogoro
2. wanafunzi walitembelea mbuga za wanyama za mikumi serengeti na ruaha
3. lo mtoto ameanguka
4. shambani kwenu kuna mazao gani
5. bibi alisema karibu mjukuu wangu



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 34 23/07/2021 14:18

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Soma habari hii, kisha jibu maswali.

## Kituo cha afya

Mimi ninaitwa Luka. Kaka yangu anaitwa Kizenga. Tunaishi katika Kijiji cha Kwale. Katika kijiji chetu kuna kituo cha afya. Siku moja niliugua mafua makali na kikohozi. Baba akaniuliza, "Umeanza lini kukohoa?" Nikamjibu, "Nilianza kukohoa tangu jana jioni". Baba akamwambia kaka, "Kizenga mpeleke Luka kwenye kituo cha afya akatibiwe". Kaka aliponiona alishangaa akasema, "Lo! Kumbe unaumwa sana? Pole sana mdogo wangu. Twende kwenye kituo cha afya ukatibiwe".




Tulipofika kwenye kituo cha afya, tuliwakuta wagonjwa wengi. Baada ya muda, muuguzi alituita na kutupeleka katika chumba cha daktari. Mimi na kaka tuliingia kwa daktari. Tulipofika kwa



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 35 23/07/2021 14:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

daktari, nilimueleza jinsi ninavyoumwa. Daktari akaniuliza, “Ulianza kukohoa lini?” Nikamjibu, “Nilianza kukohoa jana jioni”. Daktari alinipima, kisha akaniandikia dawa. Baada ya kupata matibabu, mimi na kaka tulirudi nyumbani. Hali yangu iliendelea kuwa nzuri na watu wote walifurahi.

## Maswali

1. Taja alama za uandishi zilizojitokeza katika habari hii.
2. Je, ni alama gani za uandishi zimejitokeza mara nyingi zaidi?
3. Je, ni alama gani zimejitokeza mara chache?
4. Je, herufi kubwa imetumika wapi?

## Zoezi la 5

Rudia kusoma habari ya Kituo cha afya kwa kuzingatia alama zote za uandishi.

## Zoezi la 6

Soma hadithi ifuatayo, kisha inakili katika daftari lako. Andika alama za uandishi na herufi kubwa kwa usahihi.

amani anaishi na bibi yake katika kijiji cha kilole. anamsaidia bibi yake shughuli za nyumbani. anamsaidia kusafisha nyumba kupika kuosha vyombo na kufua.
juzi amani alimuuliza bibi yake, bibi unajua kusoma bibi akajibu ninajua kusoma na kuandika. amani akasema sawa bibi kesho nitaleta kitabu changu ili tusome pamoja.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 7

**Imla**

Sikiliza kwa makini habari atakayokusomea mwalimu, kisha iandike katika daftari lako kwa usahihi.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Sita


## Taarifa za matukio mbalimbali

Ukijifunza sura hii utaweza kutoa taarifa kuhusu matukio mbalimbali. Pia, kutoa taarifa kwa kuzingatia wakati uliopo, uliopita, ujao na timilifu.


**Kutoa taarifa kuhusu ajali ya kuanguka kutoka juu ya mti**

Tazama picha hizi, kisha jibu maswali.

1.



2.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3.




4.



5.



6.




## Maswali

1. Elezea tukio linaloonekana katika kila picha kuanzia namba1 hadi 6.
2. Simulia habari nzima inayotokana na picha hizo kwa kutumia wakati uliopita.
3. Habari hiyo inatufundisha nini?



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 39 23/07/2021 14:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1

1. Soma maneno yafuatayo kwa sauti.

| | | |
|---|---|---|
| (a) alimpeleka | (b) alimbeba | (c) alikimbia |
| (d) alichuma | (e) aliokota | |

2. Maneno hayo yapo katika wakati gani?
3. Tunga sentensi moja kwa kila neno.

## Kutoa taarifa kuhusu ajali ya baiskeli

Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali.

### Ajali ya baiskeli



FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 40 23/07/2021 14:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Siku ya Jumatatu, Imani aliamka mapema kwenda shuleni. Njiani alikuta ajali ya mtu aliyeanguka na baiskeli. Alipoangalia kando ya barabara, alimuona mtu amelala chini. Alipoangalia pembeni yake, aliona tenga la nyanya na baiskeli. Usukani na gurudumu la mbele la baiskeli vilikuwa vimepinda. Baadhi ya nyanya zilizokuwa kwenye tenga zilikuwa zimesambaa barabarani. Imani alimuuliza kijana aliyeitwa Buheri,"Kaka kumetokea nini hapa?"

Yule kijana akamjibu,"Kumetokea ajali, mwendesha baiskeli ameteleza na kuanguka". Imani alisikitika sana. Akauliza tena, "Je, ameumia?" Yule kijana akamjibu, "Sina uhakika ila amepoteza fahamu". Imani akauliza tena, "Mbona hamumpeleki hospitali?" Yule kijana akajibu, "Ajali imetokea sasa hivi".

Imani aliendelea na safari yake ya kuelekea shuleni. Mbele kidogo alikutana na mwendesha pikipiki. Alimsimamisha na kumueleza kuhusu mwendesha baiskeli aliyepata ajali.

Akamuomba kama anaweza kwenda kumsaidia.Yule mwendesha pikipiki alikubali, akaenda eneo la tukio. Alipofika alimkuta majeruhi ameshapata fahamu. Watu walisaidiana na mwendesha pikipiki kumpakia majeruhi na kumpeleka hospitalini.

Siku iliyofuata walimu na wanafunzi walipata taarifa kuhusu msaada aliotoa Imani. Walimu walimuita Imani mbele ya wanafunzi wenzake na kumpongeza kwa kitendo alichofanya. Imani alifurahi sana.

## Maswali

1. Nani aliamka mapema kwenda shuleni?
2. Ajali iliyotokea barabarani ilikuwa ni ya nini?
3. Nani aliulizwa na Imani kuhusu kilichotokea?
4. Unafikiri ni kwa nini Imani aliamua kutoa taarifa ya ajali ya baiskeli?



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 41 23/07/2021 14:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. Je, Imani ni mwanafunzi mwenye tabia gani?
6. Kwa nini Imani alipongezwa na walimu wake?
7. Ukiona tukio la ajali unatakiwa kufanya nini?
8. Elezea ajali yoyote unayoifahamu au uliyowahi kuisikia.

## Zoezi la 2

Andika maana za maneno ya kifungu A kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kifungu B.

| Kifungu A | Kifungu B |
|---|---|
| (a) Poteza fahamu - | (i) mtu aliyeumia au kujeruhiwa |
| (b) Tukio - | (ii) zimia kwa sababu ya ugonjwa au ajali |
| (c) Majeruhi - | (iii) jambo lenye madhara linalotokea ghafla |
| (d) Ajali - | (iv) jambo lililotokea |
| | (v) mtu aliyelala fofofo |

FOR ONLINE USE ONLY

## Kutoa taarifa kwa kutumia wakati uliopo -na-

## Zoezi la 3

Soma sentensi zifuatazo, kisha jibu maswali.

(a) Mama anakwenda sokoni kununua mchele na unga.
(b) Mwalimu anaandika mazoezi ya Kiswahili ubaoni.
(c) Shangazi anatuimbia wimbo mzuri.
(d) Mwanafunzi anasoma kitabu cha hadithi.

Je, sentensi (a) hadi (d) ziko katika wakati gani?



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 42 23/07/2021 14:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4

Badili sentensi zifuatazo ziwe katika wakati uliopo.

(a) Mimi na mdogo wangu tulifanya usafi wa mazingira.
(b) Askari walicheza gwaride uwanjani.
(c) Mjomba aliishi kwenye nyumba ya ghorofa.
(d) Paka alikunywa maziwa.
(e) Kaka alitengeneza kiti.

## Kutoa taarifa kwa kutumia wakati ujao -ta-

## Zoezi la 5

Badili sentensi zifuatazo ziwe katika wakati ujao.

**Mfano** Mwanafunzi anafagia darasa
Mwanafunzi a**ta**fagia darasa

1. Dada anaosha vyombo.
2. Bibi alikwenda shambani.
3. Simba ananguruma msituni.
4. Baba yangu anapaka rangi nyumba yetu.
5. Wanafunzi wamefaulu mtihani.

## Kutoa taarifa kwa kutumia wakati uliopita hali timilifu -me-

## Zoezi la 6

Badili sentensi zifuatazo ziwe katika wakati uliopita hali timilifu.

**Mfano** Roda anafagia uwanja.
Roda a**me**fagia uwanja.

1. Tutaenda kumsalimia shangazi.
2. Ng'ombe anaingia zizini.
3. Paka alikamata panya.
4. Baraka atakimbia mchakamchaka.
5. Mwalimu wetu anafundisha vizuri.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 7

Tazama picha hizi, kisha toa taarifa ya kitendo kinachofanyika katika kila picha.

**Mfano**

1. Mama anashona nguo kwa cherehani.

1.




2.



3.



4.





Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 44 23/07/2021 14:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5.



6.



FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 8**

1. Andika majibu ya vitendawili hivi.
   (a) Anajua kuchora ingawa hajui anachokichora ..........
   (b) Rafiki yangu ni mharibifu lakini ninamuhitaji ..........
   (c) Anabeba mishale kila anapokwenda .............
   (d) Wazee wawili wanashuka mlima .............
   (e) Anamfundisha mzungu kutengeneza mwavuli .........
2. Vitendawili (a) hadi (e) vipo katika wakati gani?
3. Tega na tegua vitendawili vitatu unavyovifahamu.

## Kutoa taarifa kuhusu wanafunzi wasiokwenda shuleni

Soma habari hii, kisha jibu maswali.

### Kusoma ni haki yetu


Kayande ni mwanafunzi wa darasa la tatu. Anasoma katika Shule ya Msingi Juhudi. Rafiki yake anaitwa Jema. Mdogo wake Jema anaitwa Furaha. Furaha anasoma darasa la pili.

Siku moja, Kayande aliamka mapema ili awahi kwenda shuleni. Alipokuwa njiani, alikutana na rafiki yake Jema pamoja na mdogo wake Furaha. Jema na Furaha walikuwa wanachunga ng'ombe. Kayande aliwauliza, "Leo hamuendi shuleni?" Jema alijibu, "Ndiyo hatuendi. Baba ametuambia tukachunge ng'ombe. Yeye anakwenda kwenye mkutano". Kayande aliwaambia, "Si vyema kukosa kwenda shuleni. Kusoma ni haki yetu".

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Shuleni mwalimu aliita majina. Jina la Jema lilipoitwa, Kayande alijibu, "Amekwenda kuchunga ng'ombe". Mwalimu na wanafunzi walisikitika. Mwalimu akasema, "Mwanafunzi asipofika shuleni anakosa haki yake ya kupata elimu na atakuwa mjinga". Mwanafunzi mmoja alimuuliza mwalimu, "Haki za mtoto ni zipi?" Mwalimu akajibu, "Kila mtoto ana haki ya kusoma, kupendwa na kusikilizwa". Mwalimu aliendelea kusema kuwa, "Mwanafunzi anapohudhuria shuleni hujifunza mambo mengi. Pia ataweza kujiamini na kufanikiwa katika maisha yake".



Mwanafunzi mmoja alimuuliza mwalimu, "Wazazi wakituzuia kuja shuleni tufanye nini?" Mwalimu akajibu, "Mnatakiwa kuwaagiza wenzenu kutoa taarifa hapa shuleni". Kayande alimuuliza tena mwalimu, "Je, wazazi hao watafanywa nini?" Mwalimu akajibu, "Wataitwa shuleni kujieleza. Aidha, wataelezwa umuhimu wa kuwaruhusu watoto wao kuhudhuria shuleni kila siku". Wanafunzi wote walifurahi kusikia maneno ya mwalimu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maswali

1. Nani anasoma darasa la tatu?
2. Rafiki yake Kayande anaitwa nani?
3. Kwa nini Jema na Furaha hawakwenda shuleni?
4. Mwanafunzi akienda shuleni kila siku atapata faida gani?
5. Watoto wana haki gani?
6. Mzazi wako akikuzuia kwenda shuleni utafanya nini?
7. Habari hii inakufundisha nini?

## Zoezi la 9

1. Oanisha maneno na maana zake.

**Mfano**

Shule - Mahali ambapo wanafunzi hupata elimu

| Maneno | Maana |
|---|---|
| (a) Haki - | (i) peleka mifugo kula majani na kuwalinda |
| (b) Chunga - | (ii) kitu ambacho mtu anapaswa kukipata |
| (c) Mjinga - | (iii) mtu asiyejua kitu au jambo |
| (d) Shule - | (iv) mahali ambapo wanafunzi hupata elimu |

2. Tunga sentensi moja kwa kila neno.

**(a) haki** **(b) chunga** **(c) mjinga**

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Saba

## Kuelezea wanyama na wadudu


Ukijifunza sura hii utaweza kutaja kwa ufasaha majina ya wanyama na kuelezea wanakoishi. Aidha, utaweza kuelezea sifa na tabia mbalimbali za wadudu. Vilevile, utasoma kifungu cha habari na kujibu maswali.

### Kutaja majina ya wanyama na kuelezea wanakoishi

Kuna aina kuu mbili za makundi ya wanyama. Makundi hayo ni wanyama wafugwao na wanyama wa porini.

**Zoezi la 1**

1. Taja majina ya wanyama hawa.



FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 49 23/07/2021 14:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Soma na fumbua mafumbo haya.

**Mimi ni nani?**

(a) Ninakupatia nyama, maziwa na pesa. Ngozi yangu hutumika kutengenezea ngoma na mikanda. Ninatoa sauti moooo! Je, mimi ni nani?

(b) Ni mkubwa kuliko wanyama wote mwituni. Nina mkonga mrefu na masikio makubwa. Watalii husafiri kuja kuniona. Je, mimi ni nani?

(c) Ni rafiki wa binadamu. Ni mkali, nalinda nyumba na ninafukuza wezi. Ninabweka wu, wu, wu, wu! Je, mimi ni nani?

(d) Ni rafiki wa binadamu. Ni mpole, ninapenda kukaa jikoni. Ninapenda kula samaki na kunywa maziwa. Ninawinda panya. Je, mimi ni nani?

(e) Nina shingo ndefu kuliko wanyama wote wa mwituni. Ninapenda kula majani ya juu ya miti. Ninatembea kwa maringo. Ni kivutio cha watalii. Picha yangu imewekwa katika noti za Tanzania. Je, mimi ni nani?

(f) Ninaishi mwituni. Ngozi yangu ina mistari myeupe na myeusi. Watu hufurahi wanaponitazama. Je, mimi ni nani?

(g) Ninaishi majini kwenye mito, maziwa na nchi kavu. Nina mdomo mkubwa na meno mengi makali. Ngozi yangu hutumika kutengenezea mapambo. Ninafanana na kenge ingawa nimemzidi ukubwa. Je, mimi ni nani?

(h) Ninaishi kwenye miti porini. Ninakula mazao ya binadamu. Nina tabia ya kurukia miti. Ninabeba wanangu mgongoni ninapotembea. Nina mkia mrefu. Je, mimi ni nani?

(i) Ninaishi porini. Ninapenda kula mizoga. Je, mimi ni nani?

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 51 23/07/2021 14:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 2**

Igiza mafumbo ya **mimi ni nani?** katika zoezi la 1.


**Zoezi la 3**

1. Taja wanyama wengine watano unaowafahamu. Kwa kila mnyama eleza muonekano na sifa zake.
2. Chora picha ya mnyama mmoja wa porini.
3. Chora picha ya mnyama mmoja anayefugwa.

**Kuelezea kwa ufasaha sifa bainifu na tabia mbalimbali za wadudu**

Kuna aina mbalimbali za wadudu wanaopatikana katika mazingira yetu. Aina hizo ni wadudu wanaotambaa na wadudu wanaoruka.


**Chunguza picha zifuatazo, kisha jibu maswali**







Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 52 23/07/2021 14:19


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE














## Zoezi la 4

1. Taja majina ya wadudu unaowaona katika picha.
2. Taja wadudu wanaoruka.
3. Eleza tabia za wadudu hao.
4. Taja wadudu wanaotambaa.
5. Eleza tabia za wadudu hao.



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 53 23/07/2021 14:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 5**

Jibu maswali haya.

1. Taja wadudu watatu unaowafahamu.
2. Je, wadudu hao wanatofautiana kwa mambo gani?
3. Ni wadudu gani wanapatikana katika mazingira ya nyumbani?
4. Eleza tabia za wadudu uliowataja.
5. Taja wadudu wawili na madhara wanayoleta kwa binadamu.

Soma habari hii, kisha jibu maswali.

## Daudi aumwa na nyuki





Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 54 23/07/2021 14:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Siku moja, Daudi alitoroka kwenda porini kuangalia mizinga ya nyuki. Mizinga hiyo ilikuwa ya baba yake. Alipofika katikati ya msitu, aliona wadudu mbalimbali. Aliona nyigu, panzi na siafu. Daudi hakuwaogopa wadudu hao. Aliendelea na safari hadi kwenye mizinga ya nyuki.

Alipofika kwenye mizinga, alisikia kelele za nyuki. Nyuki walivuma vuuu, vuuu! huku wakizunguka mizinga. Ghafla, nyuki wachache wakamfuata Daudi na kuanza kumzunguka. Daudi alianza kuwafukuza kwa kupunga mikono lakini nyuki waliendelea kumzunguka. Daudi aliogopa sana, alivunja tawi la mti na kuanza kuwafukuza. Nyuki walikasirika na kuanza kumuuma.

Daudi alipiga kelele na kukimbia kuelekea nyumbani. Nyuki wachache waliendelea kumfuata na kumuuma. Alipofika nyumbani, wazazi wake walimpeleka hospitalini kwani alikuwa amevimba mwili mzima. Wazazi wake walimwambia, “Nyuki hutupatia asali lakini ni wadudu hatari unapowachokoza”.

FOR ONLINE USE ONLY

## Maswali

1. Daudi aliwaona wadudu gani msituni?
2. Je, wadudu gani ni hatari zaidi kati ya wadudu aliowaona Daudi?
3. Kwa nini Daudi aliumwa na nyuki?
4. Iwapo ungeumwa na nyuki kama Daudi ungefanya nini?
5. Nyuki wana faida gani?
6. Habari hii inatufundisha nini?



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 55 23/07/2021 14:19


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 6

Tegua vitendawili vifuatavyo kwa kutumia picha **a** hadi **f**.

1. Ukoo wetu hauishiwi na safari.
2. Kafa huku akining'inia.
3. Mwanangu hunipa kitu kitamu lakini akichokozwa hutawanya watu.
4. Ana miguu ya msumeno.
5. Akijikunja anakuwa herufi o akijinyoosha anakuwa namba moja.
6. Ana mdomo lakini anauma kwa mkia.


(a)




(b)




(c)




(d)



(e)



(f)



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nane


## Kuelezea mahali vilipo vitu na watu

Ukijifunza sura hii utaweza kuelezea kwa usahihi mahali vilipo vitu na watu. Vilevile, utaweza kulinganisha ukubwa  wa vitu na watu.

### Kuelezea mahali vitu na watu walipo

Tazama picha zifuatazo, kisha jibu maswali.

1.



Mpira upo wapi?

2.




Begi lipo wapi?

3.



Msichana yupo wapi?


4.



Kikombe kipo wapi?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Soma habari hii, kisha fanya zoezi.



Amosi alikuwa **juu ya** mti akichuma maembe. Mti wa maembe ulikuwa **kando ya** nyumba yao. Mti huo ulikuwa na maembe mengi sana. Ulikuwa na maembe mabichi na yaliyoiva. Amosi alichuma maembe yaliyoiva na kuyadondosha chini. Lulu na Kiba walimsaidia kuokota maembe na kuyatia **ndani ya** ndoo. Walipomaliza kuokota maembe yaliyokuwa **chini ya** mti, waliingia ndani. Walipofika ndani, waliyaosha na kuyapanga **ndani ya** kabati.

## Zoezi la 1

Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno haya.

(a) ndani ya (b) juu ya (c) chini ya (d) kando ya

1. Amosi alikuwa...........mti akichuma maembe.
2. Mti wa maembe ulikuwa............nyumba.
3. Lulu na Kiba walitia maembe............ndoo.



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 58 23/07/2021 14:19


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Tazama picha zifuatazo, kisha fanya zoezi.


1.



2.



3.



## Zoezi la 2

Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutazama picha.

**Mfano**

Basi limesimama nyuma ya lori.

1. Lori limesimama .................. basi.
2. Hamisi yupo .................. Upendo.
3. Upendo yupo .................. Hamisi.
4. Mbuzi yupo .................. ng'ombe.
5. Ng`ombe yupo ............... mbuzi.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 3**


Andika **NDIYO** kwenye sentensi ya kweli na **HAPANA** kwenye sentensi isiyo ya kweli.

1. Ndege hukaa juu ya mti. ____________
2. Wanafunzi hukaa ndani ya viti. ____________
3. Maua hupandwa kando ya nyumba. ____________
4. Ng`ombe huishi ndani ya maji. ____________
5. Binadamu huishi ndani ya nyumba. ____________

## Kulinganisha watu na kulinganisha vitu

### Kulinganisha watu

Tazama picha hizi, kisha fanya zoezi.







FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE




## Zoezi la 4

Kamilisha sentensi kwa kutumia maneno haya.

| | | |
|---|---|---|
| (a) mrefu | (b) mfupi | (c) mkubwa |
| (d) mdogo | (e) mwembamba | (f) mnene |


1. Bibi ni ......................... kuliko babu.
2. Babu ni ...................... kuliko bibi.
3. Kaka ni ...................... kuliko dada.
4. Dada ni ...................... kuliko kaka.
5. Amani ni .................... kuliko Linda.
6. Linda ni ...................... kuliko Amani.


FOR ONLINE USE ONLY


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


## Kulinganisha vitu

Tazama picha hizi, kisha fanya zoezi.









### Zoezi la 5

Kamilisha sentensi kwa kutumia maneno haya.

| | | | |
|---|---|---|---|
| (a) dogo | (b) ndefu | (c) fupi | (d) ndogo |
| (e) kubwa | (f) kidogo | (g) nene | |

1. Birika ni .................... kuliko kikombe.
2. Kikombe ni .................... kuliko birika.
3. Chupa ya chai ni ................kuliko chupa ya dawa.
4. Tikiti maji ni .................... kuliko chungwa.
5. Kamba ni .................... kuliko uzi.
6. Chungwa ni .................... kuliko tikitimaji.



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 62 23/07/2021 14:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 6

Tazama picha zifuatazo, kisha jibu maswali kwa kila picha.

1.



Wanafunzi wapo wapi?

2.



Wanunuzi wapo wapi?



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 63 23/07/2021 14:19


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3.



Wavuvi wapo wapi?

4.



Ngedere yupo wapi?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tisa

## Siku za juma

Sura hii itakuwezesha kueleza siku za juma kwa mfuatano wake. Vilevile, utaweza kuelezea shughuli zinazofanyika katika siku hizo na kuhusisha tarehe na siku za juma.

### Kuelezea siku za juma kwa mfuatano

Kuna siku saba katika juma. Siku hizo huwa katika mfuatano wake.

Tazama picha hii, kisha jibu maswali.



FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Maswali**

1. Chora na uzipange siku za juma katika mfuatano wake. Anza na Jumatatu.
2. Kuna siku ngapi katika juma?
3. Ni siku zipi za juma unazokwenda shuleni?
4. Je, unakwenda shuleni siku za Jumamosi na Jumapili?

**Zoezi la 1**

1. Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa mpangilio sahihi wa siku za juma.
   (a) Jumatatu,...................., Jumatano.
   (b) ...................., Jumamosi.
   (c) Jumanne, ....................
   (d) ...................., Ijumaa.
   (e) Ijumaa, Jumamosi, ....................
2. Eleza shughuli unazofanya siku ambazo huendi shuleni.
3. Eleza shughuli unazofanya siku ambazo unakwenda shuleni.

## Kuelezea tarehe na siku za juma

**Maswali**

Tibu maswali haya.

1. Leo ni tarehe ngapi?
2. Jana ilikuwa tarehe ngapi? Ilikuwa siku gani?
3. Keshokutwa itakuwa tarehe ngapi? Itakuwa siku gani?

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 66 23/07/2021 14:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2

Tazama kalenda hii, kisha jibu maswali.

| AGOSTI 2018 | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jumatatu** | **Jumanne** | **Jumatano** | **Alhamisi** | **Ijumaa** | **Jumamosi** | **Jumapili** |
| | | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 |
| 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 |
| 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 | 26 |
| 27 | 28 | 29 | 30 | 31 | | |

1. Hii ni kalenda ya mwezi na mwaka gani?
2. Mwezi huo ni wa ngapi katika mwaka?
3. Tarehe 15 - 8 - 2018 ni siku gani?
4. Tarehe 23 - 8 - 2018 ni siku gani?
5. Jumatatu ya mwisho wa mwezi Agosti ni tarehe ngapi?
6. Mwezi Agosti una siku ngapi za kwenda shuleni?

## Zoezi la 3

Jibu maswali yafuatayo kwa kutumia maneno **kabla ya**........ na **baada ya**..............

1. Siku inayofuata .................. Jumatatu ni Jumanne.
2. Tunanawa mikono kwa kutumia maji na sabuni .............. kuanza kula.
3. Mwezi Aprili huja .............. mwezi Machi.
4. Tunasimama mstarini .............. kuingia darasani.
5. Jumatano ni siku .............. Alhamisi.
6. Tunanawa mikono kwa sabuni .............kutoka chooni.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 67 23/07/2021 14:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Soma habari hii, kisha jibu maswali.

## Fatuma mtoto mwenye bidii

Fatuma ni binamu yangu. Anasoma Shule ya Msingi Keura. Kila siku jioni akitoka shuleni, huchukua madaftari na kujikumbusha alichosoma darasani. Vilevile, hufanya mazoezi aliyopewa na walimu wake. Siku za Jumamosi na Jumapili, Fatuma huwasaidia wazazi wake kazi za nyumbani. Pia hufua sare zake za shule.

Siku moja Fatuma alitembelewa na rafiki yake anayeitwa Tumaini. Siku hiyo ilikuwa Jumapili. Tumaini alimkuta Fatuma akifagia uwanja. Tumaini alimuuliza Fatuma kwa mshangao, "Haa! Mbona unafagia uwanja? Mimi sifanyi kazi yoyote nyumbani kwetu". Fatuma alimwambia, "Watoto tuna wajibu wa kuwasaidia wazazi wetu. Kama ulikuwa hujui, badilika kuanzia leo rafiki yangu". Tumaini alimshukuru sana rafiki yake. Alimuahidi kuwa atawasaidia kazi wazazi wake.

### Zoezi la 4

Jibu maswali haya.

1. Taja siku ambazo Fatuma haendi shule.
2. Eleza mambo anayoyafanya Fatuma siku za Jumamosi na Jumapili.
3. Taja siku ambayo Fatuma alitembelewa na rafiki yake.
4. Taja kazi ambazo Tumaini anaweza kuwasaidia wazazi wake.
5. Eleza shughuli nne unazozifanya ukiwa nyumbani.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi

# Uhusiano wa watu katika familia


Ukijifunza sura hii utaweza kuelezea uhusiano wa watu katika familia.

## Kuelezea uhusiano wa watu katika familia

Soma habari hii, kisha jibu maswali.

### Familia ya Chalo

Mimi ninaitwa Chalo. **Baba** yangu anaitwa Daudi na **mama** yangu anaitwa Anna. **Kaka** yangu anaitwa Tumaini na **dada** yangu anaitwa Sofia. **Bibi** anaitwa Chakole na **babu** anaitwa Kalonga. Mimi ni mjukuu wao. Baba ana mdogo wake anayeitwa Kimoso. Mama ana dada yake anayeitwa Jema.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Jana **mjomba** Juma alikuja kutusalimia. Leo asubuhi **shangazi** Sara amekuja kutusalimia. Amekuja na mtoto wake anayeitwa Kandida. Kandida ni **binamu** yangu. Mimi na Kandida tutacheza pamoja.

## Zoezi la 1

Jibu maswali ya kutambua uhusiano wa wanafamilia ya Chalo.

1. Tumaini anamwitaje Sofia?
2. Tumaini anamwitaje Kalonga?
3. Sofia anamwitaje Juma?
4. Tumaini anamwitaje Chakole?
5. Kandida anamwitaje Chalo?
6. Sofia anamwitaje Sara?
7. Kimoso anamwitaje Daudi?
8. Tumaini anamwitaje Jema?
9. Sofia anamwitaje Kimoso?

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la 2

Taja majina ya watu katika familia yako.

**Mfano**

1. **Mjomba** wangu anaitwa Msoke.



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 70 23/07/2021 14:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3

Kamilisha sentensi za kifungu A kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kifungu B.

| Kifungu A | Kifungu B |
|---|---|
| 1. Dada wa baba yako unamwita - | (a) baba |
| 2. Mzazi wako wa kike unamwita - | (b) kaka |
| 3. Mtoto wa mjomba wako unamwita - | (c) shangazi |
| 4. Mkubwa wako wa kike unamwita - | (d) mama mdogo |
| 5. Kaka wa mama yako unamwita - | (e) mjomba |
| 6. Mzazi wako wa kiume unamwita - | (f) bibi |
| 7. Mdogo wa kike wa mama yako unamwita - | (g) shemeji |
| 8. Kaka yake baba yako unamwita - | (h) binamu |
| 9. Ndugu yako mkubwa wa kiume unamwita- | (i) mama |
| 10. Mama wa baba yako unamwita - | (j) wifi |
| 11. Baba wa mama yako unamwita - | (k) babu |
| | (l) baba mkubwa |
| | (m) dada |
| | (n) mjukuu |

## Zoezi la 4

1. Chora picha za watu wanne wa familia yako.
2. Chini ya kila picha andika jina la uhusiano.
   **Mfano** baba, mama.

## Zoezi la 5

**Imla**

Sikiliza habari atakayokusomea mwalimu, kisha uiandike katika daftari lako.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Moja

## Shughuli za kila siku

Ukijifunza sura hii utaweza kuelezea shughuli zinazofanyika kila siku. Utaweza kuelezea shughuli hizo kwa kutumia hali ya mazoea. Vilevile, utasoma na kutunga habari fupi kuhusu shughuli zinazofanyika kila siku.

### Kuelezea shughuli zinazofanyika kila siku

Soma sentensi zifuatazo kwa sauti.

1. Kila siku asubuhi mama hupika chai.
2. Shangazi husoma kitabu cha hadithi kila siku jioni.
3. Kila siku jioni kaka huosha vyombo.
4. Mimi husoma kitabu kila siku jioni.
5. Mjomba hupenda kuvaa nguo nyekundu kila mara.
6. Kila siku usiku bibi hutusimulia hadithi.
7. Dada hufanya mazoezi kila siku asubuhi.
8. Sisi husafisha mazingira ya nyumbani kwetu kila wiki.
9. Kila Alhamisi Faraja huvaa nguo za michezo.
10. Mtoto huyu hupenda kulia kila mara.

Jibu maswali haya.

1. Huwa unafanya nini kila siku asubuhi?
2. Taja na eleza shughuli unazofanya kila Jumamosi.
3. Wazazi au walezi wako wanafanya nini kila Jumamosi?

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 72 23/07/2021 14:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1


Tunga sentensi sita sahihi kwa kutumia maneno ya kifungu A, B na C.

| Kifungu A | Kifungu B | Kifungu C |
|---|---|---|
| Kila siku mwalimu | hucheza | mazoezi ya viungo |
| Kila mara dada | hufundisha | wanafunzi darasani |
| Kila jioni kaka | hufanya | mpira wa miguu |

## Kusoma habari kuhusu shughuli za kila siku

Soma habari hii, kisha jibu maswali.

Sisi tunaishi katika Kijiji cha Dingalo. Hapa kijijini basi **hu**ondoka na kurudi kila siku. Basi hilo linaitwa Lipayo. Lipayo **hu**anza safari yake kila siku alfajiri. Likikaribia kituoni, **hu**piga honi kwa nguvu. Wasafiri **hu**lisubiri basi kituoni. Wale wanaochelewa **hu**kimbia ili kuliwahi.








FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Watu **hu**kaa kwenye viti mapema, kisha basi **hu**ondoka kuelekea mjini. Basi linapofika mjini, watu wote **hu**shuka na kuendelea na shughuli zao. Dereva **hu**peleka basi kwenye kituo cha mafuta na **h**ujaza mafuta. Baada ya kujaza mafuta, **hu**lirudisha kituoni. Watu wanaokwenda kijijini **hu**anza kupanda kwenye basi. Kondakta **hu**ingia na **hu**pokea nauli, kisha **hu**toa tiketi.

Ikifika saa nane, Lipayo **hu**anza safari ya kurudi kijijini. **Hu**beba mizigo mingi ya madukani na mingine ya abiria. Lipayo linapofika karibu na kituo cha kwetu, **hu**piga honi. Watu wengi huenda barabarani kupokea wageni wao. Wengine **hu**enda kupokea mizigo yao iliyoletwa na basi. Tukifunga shule, mimi na dada tutasafiri kwa Lipayo kwenda mjini kumsalimia kaka.

## Maswali

1. Basi linalotoka Dingalo linaitwaje?
2. Basi hilo husafiri siku zipi?
3. Lipayo likikaribia kituoni hufanya nini?
4. Kwa nini Lipayo huondoka mapema sana kijijini?
5. Chora picha ya basi hilo likiwa linasafiri kurudi kijijini.
6. Wewe umewahi kusafiri kwa basi? Ulikwenda wapi? Uliona nini njiani?

## Zoezi la 2

Andika **NDIYO** kwenye sentensi ya kweli na **HAPANA** kwenye sentensi isiyo ya kweli.

1. Lipayo hutoka kijijini mchana. ____________
2. Basi hubeba mizigo ya madukani tu linapotoka mjini. ___________
3. Basi likifika kituoni kondakta huwaita wasafiri.__________



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. Basi likitoka kijijini linakuwa tupu. ____________
5. Basi la Lipayo hujaza abiria kila siku. ____________

## Kutunga habari fupi kuhusu shughuli zinazofanyika kila mara

### Zoezi la 3

**Shughuli za kila siku za Jamali, Hamisi na Rehema.**

Panga sentensi hizi kwa mfululizo sahihi ili kupata habari.

1. Jamali, Hamisi na Rehema wanasoma darasa la tatu.
2. Hutandika vitanda vyao, huoga na kuvaa sare za shule.
3. Hunywa chai na huenda shuleni.
4. Husimama mstarini na kuingia darasani.
5. Huamka mapema kila siku asubuhi.
6. Baada ya masomo hurudi nyumbani.
7. Hufagia darasa lao na uwanja wa shule.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 75 23/07/2021 14:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Mbili

## Maneno yenye maana sawa na kinyume chake

Ukijifunza sura hii utaweza kutumia maneno yenye maana sawa katika sentensi. Vilevile, utaweza kuandika kinyume cha maneno.

### Kutaja maneno yenye maana sawa

Neno lenye maana sawa ni neno ambalo maana yake inakaribiana sana na neno au maneno mengine.

**Mfano**

Tamati - mwisho

Teremka - shuka

Chagua maneno yenye maana sawa na kuyaweka pamoja.

**Mfano**

gari – motokaa

| | | | |
|---|---|---|---|
| (a) gari | (b) kauzu | (c) pipi | (d) nyanya |
| (e) peremende | (f) dagaa | (g) bibi | (h) motokaa |

Soma hadithi hii, kisha jibu swali.

Hapo zamani za kale, palikuwa na marafiki wawili. Marafiki hao ni **Ndovu** na Mbogo. Marafiki hao walipendana sana. Walishirikiana katika shughuli zao za kila siku. Siku moja Ndovu alipanga safari ya kumtembelea **nyanya** yake kijiji cha

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

jirani. Ndovu alikwenda **gulioni** na kumnunulia nyanya yake zawadi. Zawadi hiyo ilikuwa ni **dagaa** na **jamvi. Mbogo** naye alimchumia maembe **Ndovu** kwa ajili ya zawadi. Siku ya safari, marafiki wawili waliamka mapema. Walisaidiana na kuweka vitu kwenye **motokaa.** Mbogo alilazimika kubaki ili kulinda mazao yao yasiharibiwe na **tumbili.** Ndovu alipofika kijijini alikuta nyanya yake amepika **ubwabwa** na mboga za majani. Ndovu na nyanya yake waliketi juu ya jamvi na kula pamoja. Ilipofika jioni Ndovu alifunga safari kurudi kijijini kwake. Nyanya alimpa zawadi ya **peremende**. Ndovu alicheka sana.

## Zoezi la 1


Andika maneno yenye maana sawa na yaliyowekwa rangi katika hadithi uliyosoma.

## Zoezi la 2

Soma sentensi zifuatazo kwa sauti.



Hili ni **gari.** Jina lingine huitwa **motokaa.**




Huyu ni **tembo.** Jina lake lingine ni **ndovu**.



FOR ONLINE USE ONLY

Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 77 23/07/2021 14:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| | |
|---|---|
|  Hizi ni **pipi.** Hupendwa sana na watoto. Vilevile, huitwa **peremende.** |    Hizi ni **hela.** Jina lingine huitwa **pesa** au **fedha.** Hutumika kununulia vitu mbalimbali. |
|  Hii ni **kalamu.** Pia huitwa **peni.** Peni ni kalamu ya wino. |  Kijana huyu ana**kwea** mnazi. Ni sawa na kusema ana**panda** kwenye mnazi. |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3

Chagua maneno kutoka **sehemu B** yenye maana sawa na maneno kutoka **sehemu A**. Kisha andika jibu sahihi.

**Mfano**


(a) Ada - karo

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| (a) Ada - | (i) jokofu |
| (b) Tamati - | (ii) maliwato |
| (c) Bafu - | (iii) keti |
| (d) Friji - | (iv) kocho |
| (e) Shamba - | (v) konde |
| (f) Kaa - | (vi) karo |
| (g) Chupi - | (vii) mwisho |

## Zoezi la 4

Andika majina mawili yenye maana sawa na picha hizi.


**Mfano**



Treni - Garimoshi
...............................................

FOR ONLINE USE ONLY


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

1. 

..............................................................

2. 

..............................................................

3. 

..............................................................

4. 

..............................................................

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 80 23/07/2021 14:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5

Oanisha maneno na maana zake.

**Mfano**

Jokofu

| Maneno | maana |
|---|---|
| 1. **Jokofu** → | (a) ada ya shule |
| 2. Maliwato | (b) chombo mfano wa kabati kinachotoa baridi na hutumika kuhifadhia vyakula |
| 3. Karo | (c) sehemu maalumu ya kuogea |
| 4. Gulio | (d) mahali penye mkusanyiko wa wauzaji na wanunuzi wa bidhaa za rejareja |
| 5. Peni | (e) malipo ya gari |
| 6. Konde | (f) sehemu kubwa ya ardhi iliyolimwa. |
| | (g) kalamu ya wino |

## Zoezi la 6

Andika maneno yenye maana sawa na maneno haya.

1. Mwisho ..................
2. Faulu ..................
3. Chooni ..................
4. Pipi ..................
5. Beseni ..................



FOR ONLINE USE ONLY

Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 81 23/07/2021 14:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 7

Andika sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yenye maana sawa na yaliyokolezwa wino.

**Mfano**

Kaka **alipanda** kwenye mti mrefu.

Kaka **alikwea** kwenye mti mrefu.

1. Wanafunzi wote waliambiwa **wakae** kwenye viti.
2. Darasa la tatu tunatumia **kalamu** kuandikia.
3. Dada alipika **dagaa.**
4. **Mbogo** ni mnyama hatari.
5. **Soko** lipo karibu na uwanja wa mpira.


## Kusoma na kuandika kinyume cha maneno

## Zoezi la 8

Tazama picha zifuatazo, kisha andika neno na kinyume chake.

**Mfano**


Mrefu - **mfupi**

1.  


FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


2.




3.



4.



5.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 9

Oanisha maneno ya sehemu A na kinyume chake katika sehemu B. Kisha andika herufi ya jibu sahihi katika mabano.

**Mfano**

Mbali - ***(e)***

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Mbali ( ) | (a) sahau |
| 2. Maskini ( ) | (b) lala |
| 3. Kumbuka ( ) | (c) chafu |
| 4. Amka ( ) | (d) tajiri |
| 5. Safi ( ) | **(e)** karibu |

## Zoezi la 10

Chagua neno lililo kinyume kutoka katika orodha hii. Kisha jaza nafasi iliyo wazi.

juu mbaya adui lala kaa bomoa ruka

| Neno | Kinyume |
|---|---|
| 1. Simama | ........................... |
| 2. Rafiki | ........................... |
| 3. Amka | ........................... |
| 4. Jenga | ........................... |
| 5. Chini | ........................... |
| 6. Mzuri | ........................... |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 11

Andika neno au kinyume cha neno katika sehemu iliyoachwa wazi.

| Neno | Kinyume |
|---|---|
| 1. Ingia | ................................... |
| 2 ................................... | sahau |
| 3. Kidogo | ................................... |
| 4 ................................... | rudi |
| 5. Kusanya | ................................... |
| 6. Polepole | ................................... |

## Zoezi la 12

Andika kinyume cha maneno yaliyokolezwa wino katika sentensi hizi.

1. Baba alipanda kwenye gari **dogo.**
2. Limbi anasoma shule iliyopo **mbali.**
3. Kitanda changu ni **kifupi.**
4. Wavuvi walivua samaki **wakubwa.**
5. Ugonjwa wa UKIMWI umeua watu **wachache.**

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Soma hadithi hii, kisha fanya zoezi linalofuata.

## Mfalme mjinga

Siku moja mfalme **mjinga** aliitisha mkutano. Wananchi wake walikusanyika kwa wakati uliopangwa. Katika mkutano huo aliwataka wananchi wake kufanya mambo yao kwa ushirikiano. Aliwataka **maskini** wote wasaidie wasiojiweza. Vilevile, aliamuru **kuvunjwa** kwa nyumba za kisasa. Mfalme **mjinga** aliwakumbusha wananchi wake **kupunguza** vyumba vya madarasa. Halafu, mfalme **mjinga** aliwahimiza wananchi wake **kung'oa** miti mbalimbali katika mazingira yao.Wananchi wote **walikasirika,** hivyo walionesha ishara ya kumuunga mkono.

### Zoezi la 13

Rudia kuandika hadithi hii kwa kuandika kinyume cha maneno yaliyowekewa rangi. Kichwa cha hadithi kiwe MFALME MWEREVU.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 86 23/07/2021 14:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Tatu


## Ndege wetu

Sura hii itakuwezesha kutambua majina mbalimbali ya ndege. Pia utaweza kuelezea sifa na tabia zao.

### Kuelezea sifa na tabia za ndege

Tazama picha zifuatazo, kisha soma maelezo yanayohusu picha hizo.

Huyu ni kuku. Kuku ni jamii ya ndege. Kuku hutaga mayai na kuangua vifaranga. Mayai ni chakula bora. Mimi napenda mayai.




Mwewe ni ndege. Mwewe huishi juu ya miti. Mara nyingi hupenda kuruka kutoka mti mmoja kwenda mwingine. Mwewe hula vifaranga vya kuku.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


Jogoo ni ndege anayefugwa. Jogoo huwika mapema asubuhi. Watu wengi huamshwa na sauti yake.



Kasuku ni jamii ya ndege. Ni ndege mwenye rangi nyingi. Anapenda kuiga sauti za binadamu. Mara nyingi hufugwa na binadamu.



Huyu ni batamzinga. Ni jamii ya ndege. Ni ndege wa porini na pia hufugwa. Ni mkubwa kuliko kuku. Ana rangi nyingi na hupenda kula samaki.



Huyu ni mbuni. Ni jamii ya ndege. Ni ndege mkubwa wa mbugani. Mbuni hawezi kuruka ila ana uwezo wa kukimbia sana. Mbuni hutaga mayai makubwa sana.




FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Huyu ni kunguru. Ni jamii ya ndege. Ana rangi nyeusi. Baadhi ya kunguru huwa na doa moja jeupe shingoni. Ndege huyu hula vyakula mbalimbali.



Huyu ni chiriku. Ni jamii ya ndege. Chiriku hula nafaka. Ana kelele nyingi.



Huyu ni bundi. Ni jamii ya ndege. Bundi ana macho makubwa. Mara nyingi huonekana usiku.



## Zoezi la 1

**Andika NDIYO** kwenye sentensi ya kweli na **HAPANA** kwenye sentensi isiyo ya kweli.

1. Batamzinga ni mkubwa kuliko kuku. __________
2. Njiwa ni mkubwa kuliko kanga. __________
3. Kunguru ni mkubwa kuliko mbuni. __________
4. Kunguru ana mdomo mfupi kuliko kasuku. __________
5. Bundi anaweza kuona gizani kuliko njiwa. __________

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Soma hadithi hii, kisha jibu maswali.

## Urafiki wa uongo



Hapo zamani za kale, kulikuwa na kuku na mwewe. Kuku na mwewe walikuwa marafiki sana. Kuku alikuwa na watoto watano na mwewe alikuwa na watoto watatu. Wote walikuwa wanapenda kucheza pamoja. Siku moja kulitokea njaa, mwewe akamwambia kuku waende porini kuwinda. Kuku alikubali na waliwaacha watoto na kuelekea porini. Watoto wa mwewe walikaa juu ya mti na wa kuku chini ya mti.



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 90 23/07/2021 14:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kuku na mwewe walianza safari. Walipokuwa njiani, mwewe alimwambia kuku kuwa amesahau manati yake. Hivyo, anarudi kuyachukua. Kumbe mwewe alimdanganya kuku.

Mwewe alianza safari ya kurudi nyumbani. Kuku alimsubiri mwewe akidhani kuwa atarudi mapema. Kuku alikaa kwa muda mrefu lakini mwewe hakurudi. Baadaye kuku aliamua kuanza safari ya kurudi nyumbani. Alipofika, alimkuta mwewe amekaa juu ya mti na watoto wake. Kuku alimuuliza, "Rafiki yangu mwewe watoto wangu wako wapi?" Mwewe akamjibu, "Nimewageuza chakula changu". Kuku alikasirika sana na kumchukia mwewe. Hadi leo kuku na mwewe ni maadui.

## Maswali

1. Nani walikuwa marafiki?
2. Kuku na mwewe walikubaliana kwenda wapi?
3. Mwewe alimdanganya nini kuku? Kwa nini alifanya hivyo?
4. Kitu gani kiliwatokea watoto wa kuku?
5. Kwa nini kuku alikasirika sana na kumchukia mwewe?
6. Hadithi hii inatufundisha nini?
7. Simulia hadithi hii kwa maneno yako mwenyewe.

## Zoezi la 2

1. Taja ndege wawili wanaopatikana katika eneo lenu.
2. Kwa kila ndege eleza rangi yake, ukubwa, anachokula na anavyojenga nyumba yake.
3. Chora picha ya ndege watatu na kuandika majina yao.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3

Andika umoja au wingi wa maneno yaliyomo katika jedwali.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Ndege | ........................... |
| 2. ........................... | viota |
| 3. ........................... | majani |
| 4. Mti | ........................... |
| 5. ........................... | mimea |
| 6. Mbuni | ........................... |
| 7. ............................. | marafiki |
| 8. Mtoto | ................................. |

## Zoezi la 4

Kamilisha sentensi kwa kutumia maneno haya.

(a) ndege (b) wanyama (c) mimea
(d) matunda (e) vyombo (f) vifaa

1. Mbuzi, kondoo, ng'ombe na simba ni ..................
2. Kanga, kasuku, kunguru na njiwa ni ..................
3. Chungwa, embe, papai na tikiti ni ..................
4. Sahani, kikombe, bakuli na kijiko ni ..................
5. Daftari, chaki, kalamu na kitabu ni ..................
6. Mwembe, mgomba na mchungwa ni ..................

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 92 23/07/2021 14:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Nne

## Shairi

Ukijifunza sura hii utaweza kusoma shairi la utunzaji wa mazingira. Vilevile, utaweza kuimba shairi hilo kwa usahihi.

### Kusoma shairi kuhusu utunzaji wa mazingira

Shairi huimbwa au kusomwa ili kufikisha ujumbe katika jamii.

**Mfano**

Ujumbe kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira.

Sikiliza kwa makini shairi la mazingira likisomwa na mwalimu.

### A. Tuyatunze Mazingira

1. Leo tumekusanyika, mazingira kuyajua,
Mama baba nawe kaka, ni vema mkasogea,
Ili nipate sikika, kisha nanyi tachangia,
Tuyatunze mazingira, pia nayo yatutunze.

2. Tukitunza mazingira, faida tajipatia,
Tutaepuka madhara, kama maradhi sikia,
Tutapata afya bora, hewa safi nakwambia,
Tuyatunze mazingira, pia nayo yatutunze.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 93 23/07/2021 14:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Miti hutusaidia, kwa mbao matunda pia,
   Kivuli hutupatia, na mvua kutuletea,
   Mmomonyoko huzuia, ardhi ipate tulia,
   Tuyatunze mazingira, pia nayo yatutunze.

4. Mazingira kuyatunza, faida tumezijua,
   Ovyo taka kuzitupa, acha acha nakwambia,
   Hili sio la mmoja, sote tuiweke nia,
   Tuyatunze mazingira, pia nayo yatutunze.

**Zoezi la 1**

1. Soma kishairi shairi lililoandikwa katika kifungu A kwa sauti.
2. Imba shairi hilo kishairi.

FOR ONLINE USE ONLY




Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 94 23/07/2021 14:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Soma habari B kuhusu utunzaji wa mazingira.

## B. Tuyatunze mazingira



Watu wote katika familia hupaswa kutunza mazingira.Tukitunza mazingira yetu tutapata faida nyingi. Tutapata hewa safi, tutaepuka maradhi na tutakuwa na afya bora. Miti hutupatia mbao, matunda, kivuli na mvua. Vilevile, miti huzuia mmomonyoko wa udongo. Tuache tabia ya kutupa takataka ovyo kwa kuwa zinachafua mazingira.

### Zoezi la 2

1. Taja faida mbili tunazozipata kwa kutunza mazingira.
2. Eleza nini kitatokea tukiishi katika mazingira machafu.
3. Wewe unafanya shughuli gani za kutunza mazingira?
4. Chora vitu vitano vinavyotumika kusafisha mazingira.
5. Eleza tofauti katika usomaji wa habari A na B.



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 95 23/07/2021 14:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3

Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuchagua neno sahihi katika maneno haya.

mazingira madhara fyeka mmomonyoko jitihada

1. ............. ni hali ya kuondolewa kwa udongo kunakosababishwa na maji au upepo.
2. ............. ni kukata miti au nyasi ili ziwe fupi.
3. ............. ni uharibifu unaosababishwa na kitu fulani.
4. ............. ni bidii ya kufanya jambo.
5. ............. ni vitu vinavyomzunguka binadamu.

## Zoezi la 4

Tunga sentensi moja kwa kila neno.

(a) ardhi (b) kivuli (c) hewa (d) matunda (e) afya

## Zoezi la 5

Andika kinyume cha maneno haya.

1. Chafu ____________
2. Hasara ____________
3. Tupa ____________
4. Tunza ____________
5. Kusanya ____________

## Zoezi la 6

**Imla**

Sikiliza habari atakayokusomea mwalimu kuhusu mazingira, kisha andika katika daftari lako.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 96 23/07/2021 14:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Tano

## Matumizi ya kamusi

Ukijifunza sura hii utaweza kuelewa mpangilio wa herufi za alfabeti za Kiswahili. Vilevile, utajifunza jinsi ya kutafuta maana za maneno mbalimbali kwa kutumia kamusi.

### Kusoma mpangilio wa herufi za alfabeti za Kiswahili

Imba wimbo huu wa alfabeti za Kiswahili.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| a | b | ch | d | e | f | g |
| h | i | j | k | l | m | n |
| o | p | r | s | t | u | v |
| w | y | z | | | | |

**Zoezi la 1**

1. Ziko herufi ngapi za alfabeti katika wimbo ulioimba?
2. Taja herufi zote za alfabeti kwa mfuatano sahihi kuanzia a hadi z.
3. Taja herufi ya mwanzo katika alfabeti.
4. Taja herufi ya mwisho katika alfabeti.
5. Taja herufi tano za mwanzo kwa mfuatano.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

6. Taja herufi iliyopo kabla ya **o**.
7. Taja herufi inayofuata baada ya **t**.
8. Ni herufi gani ipo kati ya **k** na **m**?

## Zoezi la 2

1. Andika herufi inayoanza na jina lako.
2. Taja maneno matatu yanayoanza na herufi **m**.
3. Taja maneno mawili yanayoanza na herufi **s**.

## Zoezi la 3

Panga majina haya kwa mfuatano wa alfabeti.

1. Baraka, Daudi, Ali, Charo.
2. Kiti, dirisha, meza, rula.
3. Tikiti, chungwa, embe, papai.

## Kutafuta maana za maneno kwa kutumia kamusi

Kamusi ni kitabu chenye maneno yaliyopangwa kwa alfabeti, yaliyokusanywa na kutolewa maana. Maneno katika kamusi hupangwa kulingana na makundi yenye sifa zinazofanana. Kamusi hutumiwa na watumiaji wa lugha husika.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 98 23/07/2021 14:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Soma habari hii, kisha jibu maswali.

## Tutumie kamusi

Siku moja mwalimu wa somo la Kiswahili, alisema, "Leo tutajifunza jinsi ya kutafuta maana za maneno kwa kutumia kamusi". Alisema kuwa tutaanza na neno **adabu.** Mwalimu alitupanga katika makundi, kisha alitupatia kamusi moja kila kundi.




Alituambia tufungue ukurasa wa kwanza wenye maneno yanayoanza na herufi **Aa**. Sote tulifungua kamusi. Mwalimu aliendelea kusema, "Tutafute maana ya neno **adabu**".

Mazungumzo yetu yaliendelea hivi.

| | |
|---|---|
| **Mwalimu** | Neno **adabu** linaanza na herufi gani? |
| **Subira** | Neno adabu linaanza na herufi **a.** |
| **Mwalimu** | Vizuri! Je, herufi ya pili ya neno adabu ni ipi? |
| **Raya** | Herufi ya pili ya neno adabu ni **d**. |



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 99 23/07/2021 14:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| | |
|---|---|
| **Mwalimu** | Uko sahihi! Sasa tuangalie ukurasa wenye maneno yanayoanza na herufi **a** ikifuatiwa na **d**. Ni ipi herufi ya tatu ya neno adabu? |
| **Neema** | Herufi ya tatu ya neno adabu ni **a**. |
| **Mwalimu** | Sawa! herufi inayofuata ni ipi?. |
| **Roda** | Herufi inayofuata ni **b.** |
| **Mwalimu** | Vizuri! Je, herufi ya mwisho ni ipi? |
| **Subira** | Herufi ya mwisho ni **u**. |
| **Mwalimu** | Vizuri sana! Je, mmeona neno adabu na maana yake? |
| **Wanafunzi** | Ndiyo mwalimu! |
| **Mwalimu** | Vizuri! Tueleze maana ya neno **adabu** kwa kusoma kutoka kwenye kamusi. |
| **Neema** | Adabu ni tabia njema, nidhamu na heshima. |
| **Mwalimu** | Vema! Sasa tutafute maana ya neno **mzigo**. Je, neno hilo tutalitafuta kwenye herufi gani? |
| **Roda** | Tutalitafuta kwenye herufi **m**. |
| **Mwalimu** | Vizuri! Fungua kamusi kwenye ukurasa wenye herufi **m.** Je, herufi inayofuata katika neno mzigo ni ipi? |
| **Raya** | Ni herufi **z.** |
| **Mwalimu** | Vizuri sana! Herufi nyingine zinazofuata ni zipi? |
| **Joeli** | Ni herufi **i, g** na **o.** |
| **Juma** | Mwalimu, tumeshaliona neno **mzigo**. **Maana yake ni kitu kizito kilichobebwa**. |
| **Mwalimu** | Vizuri sana! Je, nani anaweza kuniambia kamusi ni nini? |
| **Joeli** | Ni kitabu chenye maneno yaliyopangwa kwa alfabeti, kinachoeleza maana za maneno. |
| **Mwalimu** | Vizuri sana! Sasa tuendelee kutafuta maana za maneno mbalimbali kwa kutumia kamusi. |

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Darasa III 2018 April. 12.indd 100 23/07/2021 14:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Maswali**

Andika maana za maneno yafuatayo kwa kuyatafuta kwenye kamusi.

(a) mbuga (b) dereva (c) kivuli (d) ghala (e) samani

**Zoezi la 4**

Imba shairi lifuatalo, kisha jibu maswali.

Kiswahili lugha yetu, tunapaswa kuijua,
Maneno ya lugha yetu, twatakiwa kuyajua,
Ndani ya kamusi yetu, maneno kuangalia,
Kamusi ya Kiswahili, twatakiwa kutumia.

Wanafunzi tujifunze, kamusi kuitumia,
Na herufi tujifunze, vizuri kujisomea,
Vitabuni tujifunze, kamusi weza tumia,
Kamusi tuitumie, na maana kuzijua.

Kusoma kwa ufahamu, maneno tunahitaji,
Maneno kuyafahamu, na maana twahitaji,
Ni vema tukafahamu, kamusi twaihitaji,
Kamusi tuzitumie, na maana kuzijua.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Hebu kaka tutajie, neno unalolijua,
Wote tulifikirie, maana kukuambia,
Maana tukuambie, kamusi kuipitia,
Kamusi ya Kiswahili, twatakiwa kutumia.

Herufi zimeandikwa, maneno kutiririka,
Maneno yameandikwa, maana zinasomeka,
Kamusi imeandikwa, maneno yamepangika,
Kamusi ya Kiswahili, twatakiwa kutumia.

Kamusi ya Kiswahili, ni vema tukatumia
Wote tunastahili, kamusi kuitumia,
Maneno ya Kiswahili, maana tutazijua,
Kamusi ya Kiswahili, twatakiwa kutumia.

## Maswali

1. Shairi hili linahusu nini?
2. Ubeti wa shairi hili una mistari mingapi?
3. Shairi linasisitiza wanafunzi wafanye nini?
4. Kamusi ina faida gani?


**Eleza maana za maneno yafuatayo kwa kutumia kamusi.**


(a) herufi (b) kamusi (c) lugha


FOR ONLINE USE ONLY


## Other Books by
## Tanzania Institute of Education


### Standard Three





ISBN 978-9976-61-713-9

*Mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hakiuzwi*

Kiswahili Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tatu